TANGAZO LA SERIKALI NA. 467 la tarehe 14/7/2023

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128)*

## AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA WA GARI MOJA KWA MRADI WA UIMARISHAJI AFYA TANZANIA (SHIRIKA LA GESELLSCHAFT FUR INTERNATIONALE ZUSAMMENARBEIT (GIZ) GMBH) YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa wa gari moja kwa mradi wa Uimarishaji Afya Tanzania kwa Shirika la Geselleschaft fur Internationale Zusammenarbeit (Giz) GmbH) ya mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 2 Juni, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii lilioingizwa ndani ya nchi au kununuliwa nchini kabla ya kibali kupitia forodha na Shirika la Geselleschaft fur Internationale Zusammenarbeit (Giz) GmbH kwa ajili ya mradi wa uimarishaji afya Tanzania unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba msamaha katika Amri hii haujatolewa ikiwa gari litatumika kwa matumizi mengine au litahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo 4. Amri hii itafikia ukomo tarehe 2 Desemba, 2023.

---

**JEDWALI**

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Injini | Namba ya chassis | Mahali bidhaa iliponunuliwa (Ndani au Nje ya Nchi) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Cruiser 76 Hardtop 10-Seater, 5 Door | 1HZ-1016385 | JTEEB71JX0F20569 | Ndani/Nje ya Nchi |

Dodoma,
4 April, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha na Mipango*